# TUSHIRIKISHANE


## TONE la URENDO



**TOLEO LA MWEZI MARCH - 2024**

# DIBAJI:

Makala ya kwanza ya "Tushirikishane" ina habari chache kwa sababu habari nyingi tunashirikishana mara tu zinapotokea kwa njia ya mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp. Hata hivyo tujikumbushe daima kuwa Makala na machapisho rasmi yanalenga kuwa kumbukumbu ambazo zitabaki kama historia ambayo huandikwa kila siku kwa kupitia desturi ya kuweka kumbukumbu ya matukio ya kila siku katika kila nyumba ya shirika (PS n. 10). Lengo la pili la makala kama hii ni kuimarisha kifungo cha upendo ambacho ndicho kiini cha uwakfu wetu katika shirika letu kwa namna ya pekee (NT n.9), tukiamini kuwa mawasiliano huimarisha umoja na upendo.



# WAMISIONARI KUMI NA MMOJA WAPEWA DARAJA LA UPADRE
## NA MMOJA DARAJA LA USHEMASI

Jumamosi Januari 13 mwaka huu, Wamisionari kumi na moja walipewa daraja la Upadre na Mseminari mmoja daraja la Ushemasi. Tukio hilo la kihistoria lilifanyika Dodoma katika Parokia ya Malkia wa Damu Azizi - Kisasa. Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya Mkuu wa OFM, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma ndiye aliyetoa madaraja hayo. Wafuatao ndio waliopewa daraja la Upadre: Shemasi Abelhad Ismail Dimosso Mzaliwa wa Tegetero Morogoro; Shemasi Aidan Alphonce Mtui Mzaliwa wa Mbahe Aris Moshi; Shemasi Abibon Lawrent Rukiza Mzaliwa wa Kemondo Bukoba; Shemasi Appolonius Ludovick Byarugaba Mzaliwa wa Nshamba Kagera; Shemasi Bonaventure Aquiline Maro Mzaliwa wa Kishimundu Moshi; Shemasi Ernest August Shirima Mzaliwa wa Tarakea Rombo Kilimanjaro; Shemasi Gregory Ndeshillo Mzaliwa wa Mrao Rombo Kilimanjaro; Shemasi James Titus Makinda Mzaliwa wa K/Ndege Dodoma; Shemasi Joseph Richard Msumeno Mzaliwa wa Kambikatoto Chunya Mbeya; Shemasi Livinus Ndamwesiga Benedicto Mzaliwa wa Maruku Bukoba na Shemasi Revocatus Charles Gimbuya Mzaliwa wa Chamgasa Simiyu.

Mseminari aliyepewa daraja la Ushemasi siku hiyo ni Wilbrant Clodi Urio ambaye alipokelewa Shirikani rasmi na kwa daima siku ya Ijumaa Januari 12, siku moja kabla ya kupewa Ushemasi. Kwa hakika tukio hili ni la kihistoria kwa idadi ya waliopewa daraja takatifu. Idadi kubwa kama hii ilishuhudiwa kwa mara ya mwisho mwaka 2003 ambapo iliyokuwa Vikarieti ya Tanzania wa wakati huo ilishangilia idadi ya Wanashirika kumi na mmoja wakipewa daraja la Upadre mwaka huo. Katika tukio hilo hilo Wanashirika watatu wa Stigmatine walipewa daraja la Ushemasi pamoja na Shemasi Wilbrant Clodi Urio.



Baada ya kuwekwa wakfu kila padre alikwenda katika parokia yake ya nyumbani kwa ajili ya misa yake ya shukrani. Kwa sababu ya umbali kutoka sehemu moja hadi nyingine vikundi vitatu viliundwa kulingana na mikoa ya nchi ili kuwezesha ushiriki wa wanashirika wengine katika sherehe hizo.

Siku hiyo hiyo Mkuu wa Province aliwatangazia sehemu zao za Utume kama ifuatavyo:

Abelhad Ismail Dimosso – Parokia ya Mkiwa; Aidan Alphonce Mtui – John Merlini Formation House; Abibon Lawrent Rukiza – Parokia ya Old Maswa; Appolonius Ludovick Byarugaba – Parokia ya Manyoni; Bonaventure Aquiline Maro - Utume Teutonic Province; Ernest August Shirima – Parokia ya Shanwe Mpanda; Gregory Ndeshillo – Parokia ya Mkula Ifakara; James Titus Makinda – Masomo ya tasnia ya Mawasiliano SAUT, hata hivyo kwa sasa anabaki Parokia ya Kunduchi Mtongani; Joseph Richard Msumeno Parokia ya Kinda na Nyumba ya Malezi; Livinus Ndamwesiga Benedicto – Parokia ya Manyoni; Revocatus Charles - Utume Teutonic Province. Shemasi mpya Wilbrant Urio amepangiwa Parokia ya Itigi.



# UTUME WA DAMU AZIZI WAZINDULIWA RASMI JIMBONI BUKOBA

Mt. Gaspari Del Bufalo alipoanzisha Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu lengo lake kuu lilikuwa ni kueneza Upendo wa Mungu uliodhihirishwa katika tendo la Yesu kumwaga Damu yake yenye thamani kuliko vyote ili ulimwengu upate kuokolewa. Ndiyo maana toka mwanzo wa Shirika hamu ya Gaspari ilikuwa kuhakikisha lengo hilo linatimia. Ndiyo maana alisikika kila mara akisema: "natamani kuwa na ndimi elfu ili kuvuta roho za watu wote kwenye huruma ya Mungu kwa mastahili ya Damu azizi iliyomwagika Msalabani". Ndoto hiyo ya Mt. Gaspari ilitimia mwezi wa Januari 2024 katika tukio la kuzinduliwa rasmi kwa kundi la Wanautume wa Damu Azizi jimboni Bukoba.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Parokia ya Bk. Maria Mama yetu wa Fatima Itahwa Bukoba. Uzinduzi huo ulitanguliwa na Semina ya siku moja ambayo iliongozwa na Mkurugenzi wa Utume wa Walei wa Damu Azizi Pd. John Greyson Msengi akiambatana na Mwenyekiti wa Utume wa Damu Azizi kitaifa Mrs Beatha Matemu na wajumbe wawili toka baraza la uongozi wa kikundi hiki. Fr. Felix Mushobozi alikuwa beneti na shughuli hii akiwa kama 'home-boy' katika jimbo. Semina na uzinduzi huo ulifanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Januari 2024. Baada ya misa Takatifu iliyoongozwa na Fr. John Greyson, baadaye majira ya mchana ilifanyika ibada ya kumwabudu Yesu katika Damu yake Azizi. Wakati wa mlo wa mchana kulikuwa na tafrija fupi ambapo Fr. Adeltus Kamugisha ambaye ni Mkurugenzi wa Utume wa Walei jimboni Bukoba alifika kushuhudia kundi la kwanza jimboni Bukoba lenye Ibada kwa Damu Azizi ya Bwana wetu Yesu Kristo.



*Wamisionari Pd. Felix na Pd. Greyson katika picha ya pamoja na viongozi wa wanautume wa Damu Itahwa.*

Wengi watajiuliza kulikoni Utume wa Damu Azizi jimboni Bukoba? Mbona ni mbali na mahali ambapo Wamisionari wetu wanapofanya kazi? Njia za Bwana ni kamilifu na anavyopanga Mungu mipango yake hukamilika. Mwaka 2021 Bw. Vedasto Rugemalira Kamara ambaye ndiye Muasisi wa Utume hapo Parokiani Itahwa alimtembelea binti yake Asteria Kamara Rweyemamu anayeishi Makole Dodoma na akapata kuhudhuria baadhi ya semina za kundi la Utume wa Damu hapo Parokia ya Makole ndipo alipovutiwa na Roho na akawaza kujiunga yeyé mwenyewe, lakini akajitahidi kwenda kueneza habari za Tasaufi hii ya Damu Azizi katika Parokia yake ya nyumbani Itahwa. Huwezi kuamini, ila ukweli ni kwamba siku ya uzinduzi huo walikuwepo wana-Utume wapya 90. Walei hawa wamekuwa chachu kubwa ya kuenea kwa Tasaufi ya Damu Azizi ya Bwana wetu Yesu Kristu katika jimbo hata Mapadre na walei wa parokia za jirani jimboni wanatamani kueneza tasaufi hii.

Ili kuhakikisha moto huu ambao umewashwa usizimike Uongozi wa Utume huu kitaifa una mpango wa kurudi Bukoba mwaka huu kutoa Semina na hasa wakati wa Wiki la Damu Azizi kwenye mwezi July.


Ninahisi Mt. Gaspari anafurahi kwa hatua hii, kama alivyofurahi wakati Ibada kwa Damu Azizi ilipoenea katika Jimbo la Campagna Italia. Leo nahisi anasema: “Moyo wangu unafurahi kupindukia kuona Jimbo la Bukoba likizama ndani ya baharí ya huruma ya Mungu ambayo ndiyo Damu Azizi ya Mwanakondoo” (Mt. Gaspari barua n. 3806).



*Mlezi wa Utume wa Damu Taifa katika picha ya pamoja na wanautume wa Damu Itahwa.*

# TAARIFA MBALIMBALI

**Padre Francis Bartoloni, kama mnavyoelewa yupo Tanzania tangu mwezi August 2023 na anaendelea shughuli mbalimbali za utume wa Shirika. Yupo Tanzania kwa ruhusa ya Province ya Italia. Tunamshukuru sana kwa moyo wake wa kimisionari kwani kwa miezi hii michache amesaidia na kusimamia ukarabati wa nyumba zetu katika nyumba yetu ya malezi ya Mtumishi wa Mungu Yohane Merlini Miyuji. Mpaka sasa nyumba zile zote ni self-contained kama ambavyo imekuwa ndoto yetu ya siku nyingi. Tunategemea tutakuwa naye bado kwa shughuli nyingine kadhaa.**




Padre Deogratias Baharia wa Jimbo la Morogoro ambaye aliomba kujiunga nasi toka mwaka 2021, kwa sasa atafanya utume katika Parokia ya Manyoni ikiwa sehemu ya malezi yake.



Padre Emanuel Kimoruru: Baada ya kufanya utume kwa takriban miaka kumi katika Parokia ya Tegeta anahamia parokia ya Manyoni.



Padre Gaspar Baraka Ndinda: Kufuatia dharura ya Pd. Florence Kissima kwenda matibabu huko India Pd. Gaspar anakaimu uparoko wa ParokiaTegeta mpaka itakapotangazwa vinginevyo. Pamoja na mabadiliko hayo Pd. Gaspar ataendelea kuwa Mkurugenzi wa miito.



Fr. Josephat Msuya amemaliza Mkataba na CPPS Atlantic Province na Askofu wa Jimbo la St. Catherine Ontario ameomba Fr. Msuya awe Paroko kwenye Parokia ya St. Michael Archangel Dunnville.




Fr. William Mnyagatwa ambaye ni Mwanashirika wa Atlantic Province anatarajiwa kurudi Tanzania na ameomba kubaki kwa muda akifanya utume. Viongozi wake wameridhia na atafika mwezi April mwaka huu.

# JUBILEI YA DHAHABU NA FEDHA

Kama tulivyotangaziwa hivi karibuni, zifuatazo ni tarehe za sherehe za Jubilei ya Dhahabu ya Fr. Francis Bartoloni na Jubilei za Fedha ya Fr. Chrisogon Vulstan, Philbert Manyama na Evarist Lefiyo. Tarehe za Jubilei ya Fedha ya Pd. Richard Mjigwa tutajulishwa hapo baadaye:

**JUBILEI YA DHAHABU - FR. FRANCIS BARTOLONI:**




Water Project: 20 April 2024
Boko Parish: 5 May 2024
Italia: 2 June 2024

**JUBILEI YA FEDHA - FR. PHILBERT MANYAMA:**



Kisasa - 22 August 2024

**JUBILEI YA FEDHA - FR. CHRISOGON VULSTAN:**



UDOM Parish: 23 June 2024
UDOM Tiba: 28 July 2024
USERI Parish: Tutajulishwa

**JUBILEI YA FEDHA - FR. EVARISH LEFIYO:**



BOKO Parish: 3 August 2024
MANGO Parish Moshi: 31 August 2024

**MISA YA SHUKRANI KISHIRIKA - WOTE**
**MANYONI: 19 September 20214**

**"Maoni na mapendekezo juu ya toleo hili yanakaribishwa ili kuboresha habari zetu"**

Wasiliana na Pd. Felix Mushobozi, C.PP.S

P.O BOX 932 DODOMA

cppstzprovince@gmail.com

+255 653 475 366
+255 769 415 585

www.preciousbloodtz.or



C.PP.S
PROVINCE OF TANZANIA

"Tazama jinsi gani mioyo yetu inafarijika kwa fumbo la ufufuko. Haya shime salini ili nami pia nifufuke kweli na Yesu, ndio kusema niwe na maisha mapya na tamaa ya kutafuta utakatifu"

**(#2026)**

# HERINI *ya* *Pasaka*